JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

MAHIRI DEVELOPMENT PLATFORM (MADEP)

NAMBA ZA SIMU: 0678827971/0767632301

MTIHANI WA PILI WA UTAMILIFU DARASA LA SABA-JUNI 2019

SOMO : KISWAHILI

NAMBA YA MTAHINIWA : _____

JINA LA SHULE : _____

WILAYA : _____

MKOA : _____

MUDA : SAA 1: DAKIKA 30

MAELEKEZO

1. Jaza nafasi wazi hapo juu na katika karatasi ya kujibia.
2. Jibu maswali yote kwa kufuata maelekezo katika kila sehemu.
3. Chagua jibu sahii kisha siliba herufi yake katika karatasi ya kujibia OMR kwa kutumia kalamu ya risasi kuanzia swali 1 hadi 40.
4. Katika swali la 41 hadi 45 jibu maswali kwa kuandika majibu nyuma ya karatasi ya OMR.
5. Hakikisha kazi yako ni nadhifu na safi.

SEHEMU A: SARUFI

Chagua jibu sahihi kutoka kwenye machaguo kisha andika herufi ya jibu hilo kwenye mabano

1. Mbwa mwitu wamemzunguka kumlinda. Katika sentensi hii ni kifungu kipi cha maneno kimetumika kama kivumishi nomino?
   A. Kumlinda B. Mbwa C. Mwitu D. Mbwa mwitu E. Wamemzunguka [ ]
2. **Ambaye** hayupo ni ndugu yangu. Neno ambaye ni aina gani ya neno?
   A. Kitenzi B. Kiwakilishi C. Kivumishi D. Nomino E. Kielezi [ ]
3. Boni na Toni **walijibizana** kwa maneno makali nusura wapigane ngumi. Neno lililopigiwa mstari katika sentensi hii lipo katika kauli gani?
   A. Kutendeana B. Kutenda C. Kutendana D. Kutendwa E. Kutendeshana [ ]
4. Neno **binti** lipo katika ngeli ipi?
   A. U-I B. I-ZI C. U-ZI D.A-WA E. KI-VI [ ]
5. Umoja wa neno **nyayo** ni upi?
   A.Wayo B.Unyayo C.Mwayo D.Myao E.Mwao [ ]
6. Kitenzi kipi kati ya hivi vifuatavyo kinatokana na nomino **ziara**?
   A. Zaa B. Zuru C. Zara D. Zulu E. Zuia [ ]
7. Wanafunzi walikuwa wanaimba wimbo wa taifa. Katika sentensi hii neno lipi limetumika kama kitenzi kisaidizi?
   A. Wanafunzi B. Walikuwa C. Wanaimba D. Wimbo E. Wa taifa [ ]
8. "Wewe ni mwimbaji maarufu" wingi wa sentensi hii ni:
   A. Nao ni waimbaji maarufu C. Sisi ni waimbaji maarufu E. Ninyi ni waimbaji maarufu [ ]
   B. Wao ni waimbaji maarufu D. Wake ni waimbaji maarufu
9. Atoke mbele aliyepiga kelele. Hii ni aina gani ya tungo?
   A. Shurutia B. Tegemezi C. Changamano D. Sahili E. Ambatano [ ]
10. Mahali _____ pamepandwa maua panapendeza sana.
    A. Ambamo B. Ambayo C. Ambapo D. Ambako E. Ambazo [ ]
11. Baba **ana** gari zuri. Neno lilopigiwa mstari ni aina gani ya neno?
    A. Kiunganishi C. Kivumishi cha kumiliki E. Nomino [ ]
    B. Kielezi D. Kitenzi
12. Katika neno **ZUMBUKUKU** kuna aina ngapi za konsonati?
    A. Moja B. Nne C. Tano D. Sita E. Saba [ ]
13. Yupi kati ya watu hawa lazima awe mwanaume?
    A. Binamu B. Mtoto C. Ami D. Mpwa E. Shemeji [ ]
14. Kisawe cha neno **dosari** ni:
    A. Timilifu B. Pungufu C. Kasoro D. Nakshi E. Chache [ ]
15. Neno lingine lenye maana sawa na neno "sifuri" ni:
    A. Zero B. Ovyo C. Nunge D. Bure E. Zii [ ]
16. Kitabu cha kuandika kumbukumbu za matukio ya kila siku hujulikana kama:
    A. Kamusi B. Hundi C. Kumbukumbu D. Shajara E. Shajala [ ]
17. Orodha ipi ya herufi kati ya hizi zifuatazo imeandikwa kwa kuzingatia mpangilio wa alfabeti?
    A. k,s,b,m,d C. a,f,c,g,d E. p,r,s,t,u [ ]
    B. a,e,d,l,h,o D. c,d,e,f,g
18. Akisoma kwa bidii atafaulu mtihani wake. Katika neno "**akisoma**" kiambishi kipi kinaonyesha njeo?
    A. a- B. –ki C. Som- D. –a E. –ki- [ ]
19. Andika umoja wa sentensi hii. "**Madhumuni yao tumeyajua**"
    A. Dhumuni yako nimelijua C. Madhumuni yake tumeyajua E. Madhumuni yake nimeyajua [ ]
    B. Dhumuni lake nimelijua D. Dhumuni yako tumeijua
20. Alipendwa na kila mtu kutokana na **ukarimu** wake. Neno ukarimu ni aina gani ya neno?
    A. Kivumishi B. Kitenzi C. Kielezi D. Kiwakilishi E. Nomino [ ]

SEHEMU B: LUGHA YA KIFASIHI

21. Wakikua mama yao huwatupa mbali kwa kishindo. Jibu la kitendawili hiki ni:
    A. Nazi B. Boga C. Jiwe D. Mbarika E. Njegere [ ]
22. Nini maana ya nahau “kuuponda wa fisi”?
    A. Kutembea kwa miguu C. Kula mifupa E. Kula ovyo [ ]
    B. Kuzunguka mtaani D. Kuzongazonga
23. Malizia methali hii _____ uunge wajihi..
    A. Kata ulimi B. Kata mti C. Kata pua D. Kikulacho E. Njoo huku [ ]
24. Serikali ya Tanzania **imepiga marufuku** matumizi ya mifuko ya plastiki nchini. Nini maana ya nahau kupiga marufuku?
    A. Kuruhusu B. Kukataza C. Kudhibiti D. Kupoteza E. Kushauri [ ]
25. Kiota changu nimekizungushia boma la nyasi. Jibu la kitendawili hiki ni:
    A. Ulimi na meno B. Nanasi C. Macho D. Mzinga wa nyuki E. Siafu [ ]
26. Methali ipi kati ya hizi zifuatazo ina maana sawa na methali isemayo“Mdharau mwiba mguu huota tende” ?
    A. Maji ukiyavullia nguo sharti uyaoge D. usipoziba ufa utajenga ukuta
    B.Hucheka kovu asiyefikwa na jeraha E. Ukiona vyaelea ujue vimeundwa [ ]
    C. Mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu
27. Nini maana ya nahau “kulima miguu”?
    A.Kuongeza maneno katika habari C.Kuzurura E.Kulima shamba [ ]
    B.Kutembea umbali mrefu kwa miguu D.Kukatwa miguu
28. Kifungu kipi kinakamilisha methali hii? _____hubanduki.
    A. Umeshiba sana C. Umekuwa teja E. Umekuwa kiziwi [ ]
    B. Umekuwa jeta D. Umekuwa popo
29. Nahau ipi kati ya hizi zifuatazo ina maana ya **kukata tamaa**?
    A. Shika tama C. Kata kiu E. Poteza fahamu [ ]
    B. Kata shauri D. Kufa moyo
30. “Watoto wa mjomba wakiondoka hawarudi tena”. Jibu la kitendawili hili ni?
    A. Kivuli B. Kifo C. Sauti D. Maji E. Majani [ ]

SEHEMU C: USHAIRI.

Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali utakayoulizwa.

Moyo nimeushauri, lakini umekaidi,
Moyo kiburi hatari, mfano ni kama radi,
Moyo mefumbata shari, unayakwepa mradi,
Moyo u mwilini mwangu, turudi tuwe pamoja.

Uonapo yasofaa, yaache hayo matata,
Hata kama yanang’aa, mbali nayo wewe pita,
Hou ndio ushujaa, na kwa hayo hutajuta,
Moyo u mwilini mwangu, turudi tuwe pamoja.

Moyo jifunze busara, iwe ndio yako taa,
Ujitenge na ukora, mivuto hiyo kataa,
Chunguza zile ishara, zenye kuleta tamaa,
Moyo u mwilini mwangu, turudi tuwe pamoja.

MASWALI:

31. Shairi hili ni la aina gani?
    A. Tathnia B. Tathilitha C. Tarbia D. Talbia E. Tadhinia [ ]
32. Silabi zinazofanana kwa kila baada ya mizani kadhaa huitwa?
    A. Vina B. Mizani C. Urari D. Muwala E. Muamala [ ]
33. Jumla ya silabi katika mshororo wa ubeti wa shairi huitwa?
    A. Urari B. Muala C. Vina D. Mizani E. Vituo [ ]

34. “Hata kama yanang’aa” kifungu hiki cha maneno huitwa:
    A. Ukingo B. Mwandamo C. Utao D. Ukwapi E. Kipande [ ]
35. Shairi hili lina mishororo mingapi?
    A. Minne B. Nane C. Moja D. Mbili E. Kumi na mbili
36. Kichwa kinachofaa kwa shairi hili ni:
    A. Ujasiri B. Maadili C. Mtima D. Busara E. Kuepuka mabaya [ ]

SEHEMU D: UTUNGAJI

Panga sentesi zifuatazo kwa kuzipa herufi A,B,C na D ili zilete mtiririko mzuri.

37. Ukweli wa kauli hii ulijitokeza mara tu baada ya mzee Shemboko kupata uongozi. [ ]
38. Mbali na hilo, rushwa na ubadhirifu vilitawala katika kila sekta ya umma . [ ]
39. “ Umdhaniaye ndiye kumbe siye”! [ ]
40. Mzee huyo aliyatumia madaraka yake vibaya kwa kuminya haki na uhuru wa raia. [ ]

SEHEMU E: UFAHAMU

Soma kwa makini kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali kwa usahihi kama ulivyoulizwa

Kiongozi awe wa serikali au taasisi ya kidini lazima awe ni kioo cha jamii.Ili mtu awe kiongozi bora ni lazima awe mfano mzuri wa kuigwa kitabia na kimwenendo. Pia, natakiwa kufanya maamuzi ya haki na kutimiza majukumu yake bila ubaguzi wala upendeleo. Kwa kufanya hivyo atajenga imani kwa watu anaowaongoza na itakuwa rahisi kuungwa mkono na watu wake. Kiongozi bora hapimwi kwa muonekano wake ama namna anavyofoka akiwa majukwaani, bali hupimwa kwa uwezo wake wa kutimiza matakwa ya wananchi anaowaongoza.

Siku hizi imeibuka kasumba moja kwamba vijana ndiyo wanaopaswa kuaminiwa na kupewa madaraka ya kuliongoza taifa hili. Hata hivyo, umri hauwezi kuwa kigezo cha mtu kuwa kiongozi bora. Wapo vijana ambao wameaminiwa na kupewa madaraka makubwa katika nafasi mbalimbali za uongozi serikalini, lakini vijana hao wanafanya kinyume na matarajio ya walio wengi. Wengi wao wamejawa na kiburi, chuki, na hutumia madaraka waliyopewa kama nyenzo ya kuwakandamiza wengine.Wamesahau kuwa madaraka waliyonayo ni ya muda tu.

MASWALI

41. Pendekeza kichwa cha habari hii kisichozidi maneno manne_____
42. Ili mtu awe kiongozi bora anatakiwa aweje?_____
43. Kiongozi bora hupimwa kwa nini?_____
44. Kwa mujibu wa habari uliyosoma hapo juu kitu gani hakiwezi kuwa kigezo cha kiongozi bora?_____
45. Nahau kuungwa mkono kama ilivyotumika katika kifungu cha habari hapo juu ina maana gani?

    _____